

Kujiandaa kwa Mabadiliko ya Huduma za Matibabu kwa Wakimbizi

Tafadhali usi subiri hadi huduma iishe ndipo uanze kupanga Kuchukua hatua hizi sasa kunaweza kusaidia kupunguza mapengo katika huduma za matibabu na kuhakikisha upatikanaji endelevu wa matibabu na dawa zinazohitajika.

Chukua hatua zifuatazo ili kujiandaa na upotezaji wa bima ya afya:

- ☐ Panga miadi ya daktari haraka iwezekanavyo Ikiwa una mahitaji ya matibabu yana endelea, panga miadi kabla ya huduma kubadilika ili uweze kujadili mpango wako wa matibabu na daktari wako.
- ☐ Omba usambazaji wa dawa za kuandikwa na daktari za siku 90 mwezi Septemba. Ikiwa una tumiye dawa kila siku, unapaswa kumwomba daktari wako kuhusu kujazwa tena kwa siku 90 kabla ya huduma kubadilika. (Upatikanaji unategemea mpango wa afya, dawa, na idhini ya mtoa huduma.)
- ☐ Kamilisha miadi yoyote ya matibabu inayo pendekezwa. Ziara za wataalamu, miadi ya ufuatiliaji, kazi ya maabara, au huduma za kuzuia zinapaswa kupangwa sasa ikiwa inawezekana, na kukamilishwa kabla ya Oktoba 1, 2026.
- ☐ Mwombe mtoa huduma wako nakala za rekodi za matibabu Historia ya matibabu, rekodi za chanjo, orodha za dawa, na matokeo ya vipimo hufanya iwe rahisi kuanzisha huduma na mtoa huduma mpya ikiwa inahitajika.
- ☐ Anzisha huduma katika kituo cha afya cha jamii au kliniki ya ada inayo badilika kulingana na mapato. Vituo vingi vya afya vya jamii hutoa huduma kulingana na mapato. Kuwa mgonjwa aliye sajiliwa kabla ya huduma ya dharura kuhitajika.
- ☐ Endelea kutumia dawa kama ulivyo elekezwa Usi simamishe dawa kwa sababu ya wasiwasi wa gharama. Ongea na daktari au mfamasia kuhusu mbadala za bei ya chini, dawa za kawaida, au programu za usaidizi kwa wagonjwa.
- ☐ Uliza kuhusu programu za usaidizi wa dawa. Kampuni nyingi za dawa, kliniki za jamii, na mashirika yasiyo ya faida hutoa programu ambazo zinaweza kusaidia kupunguza gharama za dawa.
- ☐ Jua mahali pa kwenda kwa huduma. Tazama jedwali hapa chini.
- ☐ Sasisha maelezo ya mawasiliano. Hakikisha watoa huduma za afya na mashirika ya faida yana nambari yako ya sasa ya simu, anwani, na barua pepe.
- ☐ Weka hati muhimu pamoja. Hii ni pamoja na nakala za kitambulisho, habari za bima, rekodi za matibabu, maagizo ya daktari, na habari za mawasiliano za mtoa huduma.
- ☐ Omba mkalimani ikiwa inahitajika Wateja wana haki ya kupata usaidizi wa lugha ya bure wakati wa miadi ya matibabu.
- ☐ Endelea kuwasiliana na msimamizi wa kesi au shirika la makazi mapya. Wanaweza kukusaidia kuunganishwa na rasilimali za jamii, msaada wa kifedha, msaada wa chakula, usafiri, na watoa huduma za afya wa bei ya chini.

Mahali pa Kwenda kwa Huduma

Hali	Mahali pa Kwenda
Mahitaji ya kawaida ya matibabu	Mtoa huduma wa msingi
Ugonjwa au jeraha ambalo haliwezi kusubiri, lakini sio hatari kwa maisha	Huduma ya dharura
Dharura inayo tishia maisha	Piga simu 911 au nenda kwenye chumba cha dharura